MIRADI MBALIMBALI ILIYOTEKELEZWA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

1 UJENZI WA VITUO VYA AFYA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumla ya Tshs. 2,096,000,000.00 zimetumika katika ujenzi wa vituo vya Afya vya Ikukwa, Santilya na Ilembo kati ya fedha hizo **Tshs**. **1,700,000,000.00.** ni mapokezi ya fedha toka Serikali Kuu, Mapato ya ndani ya Halmashauri **Tshs**. **280,165,300.** Michango ya Wananchi **Tshs. 96,045,600.00** na Wahisani **Tshs. 20,000,000.**

Mchanganuo wa matumizi ya fedha katika vituo vya afya.

NA	JINA LA MRADI	SERIKALI KUU	HALMASHAURI YA WILAYA	MCHANGO WA WANANCHI	WAHISANI
1	Kituo cha Afya Ikukwa	800,000,000.00	178,254,000.00	12,600,000.00	-
2	Kituo cha Afya Santilya	500,000,000.00	64,295,700.00	17,660,600.00	-
3	Kituo cha Afya Ilembo	400,000,000.00	37,615,600.00	65,785,000.00	20,000,000.00
	JUMLA	**1,700,000,000.00**	**280,165,300.00**	**96,045,600.00**	**20,000,000.00**

2. 1 UJENZI WA KITUO CHA AFYA IKUKWA.

Kituo cha Afya Ikukwa kilipokea na kutumia Jumla ya **Tshs. 990,854,000.00** kati ya fedha hizo Serikali Kuu **Tshs. 800,000,000.00,** Mchango wa Halmashauri **Tshs. 178,254,000.00** na Wananchi **Tshs. 12,600,000.00.** Majengo yaliyojengwa ni kama ifuatavyo;

i. Jengo la wagonjwa wa nje OPD
ii. Jengo la Mama na Mtoto Kliniki
iii. Jengo la upasuaji
iv. Jengo la utawala
v. Wodi ya kina Mama wajawazito
vi. Nyumba ya mganga
vii. Nyumba ya kuhifadhia maiti na
viii. Matundu 8 ya vyoo (Me 4 na Ke 4)

Majengo yote yamejengwa na kukamilika kituo kinatoa huduma za uzazi na chanjo na huduma za wagonjwa wa nje (OPD). Aidha kituo kimepokea vifaa tiba ikiwa ni pamoja na friji,mashine ya kutakasa vifaa tiba na mashne ya joto kwa ajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya muda wake vyenye thamani ya **Tshs.12,656,700.00**

2..2. UJENZI WA KITUO CHA AFYA SANTILYA.

Ujenzi wa kituo cha Afya Santilya umegharimu Jumla ya **Tshs 581,956,300.**00 kati ya fedha hizo Serikali Kuu **Tshs.500,000,000** Mapato ya ndani ya Halmashauri ya **Tshs. 64,295,700.** Na nguvu za wananchi **Tshs 17,660,600.00,** kituo kina majengo yafuatayo;

i. Nyumba ya mganga
ii. Ujenzi wa vyoo matundu 8 (Me 4 na ke 4)
iii. Jengo la wagonjwa wa Nje (OPD)
iv. Chumba cha upasuaji
v. RCH na Wodi ya kina mama kitua cha Afya Santilya na

Majengo yote yamejengwa na kukamilika kituo kinatoa huduma mbalimbali za Afya ikiwa ni huduma za Mama na Mtoto (RCH) na uzazi.

2.3. UJENZI WA KITUO CHA AFYA ILEMBO.

Mheshimiwa Mwenyekiti Ujenzi wa kituo cha Afya Santilya umegharimu Jumla ya **Tshs. 523,400,600.00** kati ya fedha hizo Serikali Kuu **Tshs. 400,000,000.00** Mapato ya ndani ya Halmashauri **Tshs.37,615,600** na mchango

wa Wananchi **Tshs. 65,785,000.00** na Wahisani (Walter Reed) **Tshs. 20,000,000.00** .Kituo kina majengo yafuatayo;

i. Chumba cha upasuaji
ii. Wodi ya akina mama wajawazito
iii. Maabara
iv. Nyumba ya mganga
v. Nyumba ya kuhifadhia maiti na
vi. Jengo la kufulia nguo

Aidha hadi sasa jumla ya majengo manne (4) yamejengwa na kukamilika na Majengo 2 bado hayajakamilika ambayo ni Nyumba ya kuhifadhia maiti na Jengo la kufulia nguo ujenzi utakamilishwa katika Bajeti ya Mwaka 2020/2021. Kituo kinatoa huduma mbalimbali ikiwa ni upasuaji kwa akina Mama wajawazito.

3. UKAMILISHAJI UJENZI WA ZAHANATI.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya katika kipindi cha Mwaka 2015/16 hadi Mwezi Mei, 2019/20 imetumia jumla ya **Tshs 432,373,563.00** toka katika vyanzo mbalimbali; Wahisani **Tshs. 268,470,563.00,** Mapato ya ndani ya Halmashauri **Tshs. 98,951,000.00**, Michango ya Wananchi **Tshs.53,402,000.00** na Serikali Kuu **Tshs.11,550,000.00** kwa ajili ya ujenzi na ukmilishaji wa zahanati za Igoma, Isuto,Mwashoma,Songwe viwandani na Iyawaya kama inavyoonekana katika mchanganuo wa matumizi kama ifuatvyo;

i. Ukarabati zahanati ya Isuto kwa kunyanyua paa jengo la wagonjwa wa nje, kujenga sehemu ya kusubiria matibabu, kuchimba kisima, kujenga jengo la kisima na kujenga mnara wa tenki la maji ambapo kiasi cha **Tshs 83,155,250.00** kimetumika.
ii. Jumla ya **Tshs.80,373,110** zilikuwa zimetolewa toka wahisani kwa ajili ya kufanya ukarabati zahanati ya Igoma kwa kujenga njia za kupita wagonjwa "walk ways" na kujenga mfumo wa kuvunia maji ya mvua na kichomeo taka Jumla ya **Tshs 60,373,110.00** na **Tshs.20,000,000** zimetumika katika ujenzi wa jengo la kutolea huduma za CTC

iii. Ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto (**RCH**) katika zahanati ya Mjele jumla ya **Tshs.94,942,203.00** zimetumika kati ya fedha hizo Wahisani **Tshs.84,942,203.00,** Mchango wa Halmashauri **Tshs.5,000,000** na Nguvu za Wananchi **Tshs.5,000,000**

iv. Ujenzi wa zahanati katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Galijembe kiasi cha **Tshs.73,951,000.00** zimetumika fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.

v. Jumla ya **Tshs.49,952,000.00** zimetumika katika ukamilishaji ujenzi katika zahanati ya Mwashoma kati ya fedha hizo **Tshs.48,402,000.00** ni mchango wa wananchi na kiasi cha **Tshs.1,550,000.00** ni fedha toka Mfuko wa Jimbo.

vi. Ukamilishaji ujenzi zahanati ya Songwe viwandani kiasi cha **Tshs.30,000,000.00** zimetumika ,Mapato ya ndani Tshs.20,000,000.00 na Serikali Kuu **Tshs.10,000,000.00**

4. UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni miongoni mwa Halmashauri 67 zilizopata fedha kwa Mwaka 2018/2019 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya, kwa ajili ya ujenzi wa majengo 7 ya kipaumbele;

- Utawala,
- Jengo la Wagonjwa wa nje (OPD),
- Maabara,
- Mionzi (Xray),
- Jengo la kufulia
- Jengo la Wazazi (Martenity ward)
- Stoo ya dawa

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbeya umekamilika. Hadi sasa Mradi umegharimu jumla ya **Tshs 1,761,300,000.00** kwa mchanganuo ufuatao;

- Serikali Kuu Tshs .**1,500,000,000.00**
- Mchango wa Halmashauri **Tshs.64,000,000.00**
- Nguvu za Wananchi **Tshs.127,300,000.00**
- Fedha za Mfuko wa Pamoja (HSBF) **Tshs.70,000,000.00**

5. MAJI.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Vijiji (RUWASA) katika kipindi cha Miaka mitano kuanzia mwaka 2015 – 2020 imeendelea kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata Maji safi na salama. Aidha idadi ya Wananchi wanaopata Maji Safi na Salama ikiongezeka kutoka asilimia 43 Mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 58.65 Mwaka 2020.

5.1 Miradi ya Maji iliyotekelezwa katika Kipindi cha Mwaka 2015 hadi Mwaka 2020.

Aidha Katika kipindi hicho, miradi mbalimbali ya maji imetekelezwa kwa kutandaza mabomba yenye urefu wa kilometa **108.763** yaliyogharimu jumla ya **Tshs. 3,036,519,601.80** kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

MIRADI YA MAJI ILIYOTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015 - 2020

NA.	JINA LA MRADI	IDADI YA MATENKI	UREFU WA MABOMBA	THAMANI YA MRADI
1	Izumbwe/Iwindi/Mwashiwawala	3	61.213	1,510,132,760.00
2	Mradi wa Maji Mbalizi	1	-	300,000,000.00
3	Swaya/ Lupeta	1	24.898	480,691,455.00
4	Idimi/Haporoto	1	22.652	745,695,386.80
	JUMLA	**6**	**108.763**	**3,036,519,601.80**

6. IDARA YA ELIMU MSINGI.

;

6.1 ELIMU YA AWALI.

- Madarasa ya Elimu ya Awali yameongezeka kutoka 158 Mwaka 2015/2016 hadi kufikia 164 mwaka 2019/2020ikiwa ni ongezeko la Madarasa 6 katika Shule za Lunji,Pipeline,Twisa,Trinity,Godsbridge na Future.

6.2 ELIMU MSINGI.

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

i. Idara ya Elimu Msingi katika kipindi cha Mwaka 2015/2016 hadi kufikia Mwaka 2019/2020 ilikuwa imepokea toka Serikali kuu Jumla ya **Tshs.1,056,242,298** kwa ajili ya ukamilishaji vyumba vya madarasa 77 katika Shule za Msingi 62 Mwaselela 3, Ileya 3, Simambwe 3, Ilangale 2, Italazya 2, Imezu 2, Ifiga 2, Hekima 2, Haonde 2, Ifupa 2, Idiwili 2, Igalukwa 2, Igale 2, Tembela 2 Mwenge 1, Isende 1, Sanje 1, Mpande 1, Jojo 1 , Shuwa 1 ,Iyunga Mapinduzi 1, Itete 1, Shinzingo 1, Shisonta 1, Shitete 1, Nsega 1, Iwindi 1, Juhudi 1, Shongo 1,Pipeline 1, Mlimareli 1, Jitegemee 1, Mbeya Peak 1, Kawetere 1, Lwanjilo 2, Maganjo 1, Mkapa 1, Idunda 1, Tuyombo 1,Inyala 1, Darajani 1, Mwashoma 1, Iyawaya 1, Isebe 1, Nhindo 1, Ilota 1,Igunga 1, Iwanga 1 na Lunji 1.

ii. Ujenzi wa nyumba za Walimu imeongezeka kutoka 477 mwaka 2015 hadi nyumba 499 mwaka 2020 ikiwa ni ongezeko ya nyumba 22, hadi kufikia Mwezi Mei 2020 Idara ya Elimu Msingi ilikuwa imepokea jumla ya **Tshs. 85,000,000** kwa ajili ya ukamilishaji ujenzi wa nyumba za walimu 22 (Nyumba 3 kwa fedha za wahisani **Tshs.75,000,000** na nyumba ya familia mbili **Tshs.10,000,000** mapato ya ndani ya Halmashauri na Nguvu za wananchi nyumba 18) Shule zilizojenga nyumba ni Shule za Ilota, Mkapa , Ilembo , Chang`ombe, Itaga ,Shango , Mwaselela, Nsambya , Shihola, Mwakasita, Sanje , Pashungu ,Nhindo , Itega, Kawetere, Inyala, Iyawaya, Nyalwela, Mwenge, Iyunga mapinduzi , Santilya na Njelenje A.

iii.Matundu ya Vyoo yameongezeka kutoka 1,815 Mwaka 2015 hadi kufikia matundu 2,318 Mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la matundu ya vyoo 503 ambapo matundu 174 yamejengwa kwa fedha za wahisani **Tshs.322,980,069** na matundu 329 yamejengwa kwa nguvu za wananchi . katika Shule za Msingi Nywalela 21 , Shango 10 , Kikondo 14 , Ngole 13 , Izumbwe II 10, Izumbwe I 10 ,Iyawaya 15, Dimbwe 10 , Mbonile , Njelenje A 10 , Njelenje B 10 ,

Kawetere 12 , Idimi 24 , Ileya 6 , Mbeya Peak 10 , Malowe 12 , Lupeta 11 , Santilya , Iwiji 12, Ilota

11 , Nsheha 6, Nhindo 5, Sayuma 8, Sanje 10, Pashungu 8, Shihola 4, shisonta 8, Shisyete 10, Simambwe 12, Songwe II 20, Swaya 12, Tuyombo 24, , Itega 12 , Darajani 4, Horongo 7 , Idiwili 6, Ifiga 6, Ijombe juu 10 Itimba 12, Isende 12, Lusungo 18, Mapelele 18, Ndola 20, Mwampalala 12, Masoko 6 Mlimareli 18 , Imezu 12 na Chang`ombe 13.

7. ELIMU SEKONDARI.

Miradi ya Maendeleo.

Katika kipindi cha Mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020 Idara ya Elimu Sekondari imetekeleza Miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo: -

- Ujenzi wa vyumba vya maabara na ununuzi wa vifaa Umeongezeka. Maabara zimeongezeka kutoka 84 mwaka 2015 hadi kufikia 90 mwaka 2020 na vifaa vya maabara vimenunuliwa katika shule 3 za sekondari. Maabara zilizoongezeka ni sita (Galijembe – 2, Iyelanyala – 2 na Sasyaka – 2) Aidha, maabara za Sasyaka na Iyelanyala zimejengwa kwa nguvu za wananchi na za Galijembe zilijengwa kwa jumla ya **Tshs.57,333,321.02** (Mapato ya ndani **Tsh 39,089,050.02**/ Serikali Kuu Tsh 18,244,271/=)
- Samani za maabara zimenunuliwa katika shule za malama, shibolya, imezu, na santilya kwa jumla ya shilingi jumla ya **Tshs. 125,149,365.56.** Ujenzi wa vyumba vya maabara unaendelea katika shule ya sekondari Usongwe
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa umeongezeka kutoka vyumba 422 mwaka 2015 hadi kufikia vyumba 451 mwaka 2020. Jumla ya Tshs. 291,506,526.86 zimetumika. Ujenzi umefanyika katika shule za Swaya- 2, Imezu - 2 Iyelanyala - 2, Mshewe- 2, Usongwe – 4, Galijembe – 2, Isuto – 3, Malama – 4, Mpesu – 1, Songwe – 2, llembo – 2, Ilunga – 3.
-
- Kukarabati vyumba vya madarasa vyumba 14, **Tshs. 135,078,273.20** zimetumika. Ukarabati umefanyika katika shule za Ilungu madarasa 8, Nsongwijuu madarasa 2, Isuto madarasa 2 Iwiji madarasa 2.
- Ujenzi wa matundu ya vyoo kwa wanafunzi na walimu kutoka 604 mwaka 2015 hadi kufikia 648 mwaka 2020 kwa gharama ya **Tshs. 209,665,597.00.** Ujenzi wa matundu ya vyoo umefanyika katika shule za Ilungu (Matundu 14 (Shisyete(Matundu 10), Izyira(Matundu 10 - walimu 2 na wanafunzi 8) , ,Ihango - 4 na Imezu - 6
- Ujenzi wa nyumba za walimu za familia mbili (2 in 1) na familia sita (6 in 1) kutoka 55 mwaka 2015 hadi kufikia 74 mwaka 2020 kwa gharama **za Tshs.**

410,079,511.00. Ujenzi umefanyika katika shule za Shisyete 1, Sasyaka - 1, Iwiji - 1, Galijembe 1, Shibolya 1 na Izyira -1.

- Ujenzi wa hostel za wavulana na wasichana zimeongezeka kutoka 11 mwaka 2015 hadi kufikia 13 mwaka 2020. Hostel zimeongezeka katika shule ya sekondari Imezu (1) kwa nguvu za wananchi na katika shule ya sekondari Galijembe (1) kwa jumla ya shilingi **Tshs. 162,783,953.00** zilizochangiwa na serikali pamoja na nguvu za wananchi**.**

- Ujenzi wa bwalo la chakula 1 katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Galijembe Mwaka 2019/2020 kwa gharama ya **Tshs.224,811,651.98** kati ya fedha hizo serikali kuu **Tshs. 100,000,000.00** mapato ya ndani **Tshs.110,461,651.98** na nguvu za wananchi yenye thamani ya **Tshs.14,350,000.00**
- Kutengeneza meza na viti vya wanafunzi umeongezeka kutoka 13,324 mwaka 2015 hadi kufikia viti 14,480 mwaka 2020 kwenye shule zifuatazo: Ilungu Meza 200 na Viti 200, Isuto Meza 35 na Viti 35, Nsongwijuu Meza 202 na Viti 202, Imezu Meza 40 na Viti 40 Shibolya Meza 60 na Viti 60 , na Galijembe Meza 108 na Viti 108.

8. **HUDUMA ZA KIUCHUMI**

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.

- Utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu imeongezeka kutoka **Tshs. 190,000,000** mwaka 2015 kwa vikundi 66 hadi kufikia **Tshs. 621,674,000** Mwaka 2019/2020. Aidha idadi ya vikundi vilivyowezeshwa vimeongezeka kutoka vikundi 66 Mwaka 2015/2016 hadi kufikia vikundi 269 Mwaka 2019/2020 ambayo ni sawa na asilmia 308.Aidha vikundi hivi vimeweza kukuza mitaji yao na kuweza kutekeleza Miradi ya Kati yenye mlengo wa uchumi wa viwanda Mfano; Mradi wa utengenezaji sabuni unaotekelezwa na kikundi cha Mwanamke jiamini , ushonaji nguo Kikundi cha Walindu ,utengenezaji wa chaki unatekelezwa na Kikundi cha Huyandola, Mkaa mbadala kikundi cha Charcha na Miradi ya usafirishaji kwa vijana hususani Bajaji,guta na Bodaboda Kikundi cha Umwema Bodaboda na Nguvu ya Taifa.

8.1 Utoaji wa Mikopo kwa miaka mitano 2015/2016 hadi kufikia Mwaka 2019/2020

Na	**Mwaka**	**Fedha zilizotolewa**			**Jumla**	**Idadi ya Vikundi**			**Jumla y**
		Wanawake	**Vijana**	**Walemavu**		**Ke**	**Vij**	**Wal**	**Vikundi**
1	2015/16	115,000,000	75,000,000	**0**	190,000,000	43	23	0	66
2	2016/17	71,000,000	39,000,000	0	110,000,000	21	9	0	30
3	2017/18	268,500,000	166,500,000	0	435,000,000	75	33	0	108
4	2018/19	178,997,000	289,864,500	0	468,861,500	16	13	0	29
5	2019/20	202,500,000	372,552,000	46,622,000	621,674,000	20	14	2	36
JUMLA		**835,997,000**	**942,916,500**	**46,622,000**	**1,825,535,500**	**175**	**92**	**2**	**269**

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya katika kutekeleza adhima ya Serikali na kuzingatia Sheri ya Fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290 kifungu cha 37 A (4)1, ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi ya mwaka 2019 inayohusu wajibu wa Halmashauri kutenga fedha 10% toka mapato yake ya ndani na kuchangia kila mwaka kwa kutoa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Jedwali Na 4: Mchanganuo wa fedha za Mapato ya ndani 10% na fedha za mfuko zilizotolewa kuanzia 2015/2016 hadi 2019/2020:

Na	Mwaka	Fedha zilizotolewa na Halmashauri 10%				Fedha ya mfuko (Revolving)		
		KE. TSH.	VIJ. TSH.	WALEMAVU	JUMLA TSH	KE. TSH.	VIJ.TSH.	JUM
1	2015/16	25,000,000	25,000,000	0	50,000,000	90,000,000	50,000,000	140,0
2	2016/17	30,000,000	30,000,000	0	60,000,000	41,000,000	9,000,000	50,00
3	2017/18	91,500,000	91,500,000	0	183,000,000	177,000,000	75,000,000	252,0
4	2018/19	104,784,000	191,440,000	0	295,811,900	74,625,100	98,424,500	173,0
5	2019/20	92,200,000	91,865,000	46,622,000	230,687,000	110,300,000	280.687,000	390,9
JUMLA		**343,484,000**	**337,940,000**	**46,622,000**	**819,498,900**	**492,925,100**	**232,424,500**	**1,006**

8.2. PROGRAMU YA STAWISHA MAISHA

Aidha pamoja na kutekeleza zoezi hili la mpango wa kunusuru kaya masikini.Halmashauri iliteuliwa kuwa Halmashauri ya majaribio katika kutekeleza programu ya masuala ya lishe ya STAWISHA MAISHA kupitia walengwa wa TASAF.

Lengo la Programu hii ni kutoa elimu kwa Walengwa wa mpango kuhusiana na masuala ya lishe ili kupunguza lishe duni kwa wamama wajawazito na Watoto chini ya umri wa miaka mitano kwa kufanya mafunzo ya Lishe wakati wa vipindi vya asubuhi kabla ya walengwa kupokea ruzuku yao. Programu hii inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya TASAF na UNICEF katika Vijiji 105 vya Kata 28 vilivyoko kwenye Mpango wa kunusuru kaya Masikini Progaramu hii ilianza kutekelezwa tangu mwezi Oktoba 2017 hadi Januari 2019 ambapo Wawezeshaji kutoka TASAF Makao makuu walitoa mafunzo ya Programu ya STAWISHA MAISHA kwa Wawezeshaji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Wajumbe wa Kamati ya usimamizi wa Jamii.

Wawezeshaji walifanya zoezi la uundaji wa Vikundi na Jumla ya Vikundi **780** vya Walengwa wa Mpango viliundwa na kupata mafunzo ya Masuala ya Lishe siku ya Malipo ya ruzuku kwa walengwa kupitia vipindi vya asubuhi kabla ya malipo ambapo Mwezeshaji kutoka Ngazi ya Halmashauri ndiye aliyewezesha zoezi la uundaji wa vikundi

Mafunzo ya Lishe kupitia vikundi vya STAWISHA MAISHA yamefanyika katika Awamu Sita za Malipo ya ruzuku kwa Walengwa wa Mpango ambapo kila Awamu sita za Vipindi vya malipo kuanzia mwezi Machi/Aprili 2018 na kumalizika mwezi Januari /Februari 2019.

9.0 SEKTA YA KILIMO, USHIRIKA NA UMWAGILIAJI

5.1. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

5.1.1. UJENZI WA SKIMU YA UMWAGILIAJI MSHEWE

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya katika kipindi cha Mwaka 2015/16 hadi 2019/20 ilipokea Jumla ya **Tshs 250,000,000.00** toka Serikali Kuu kwa ajili kuboresha Skimu ya umwagiliaji Mshewe ili kuongeza uzalishaji na ufanisi wa matumizi bora ya rasilimali maji.

5.1.2. UKARABATI WA MAGHALA

Katika Mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri ilikuwa imetumia jumla ya **Tshs 1,369,513,516.00** kwa ajili ya kufanya ukarabati wa maghala kumi na tatu (13) katika vijiji vya Idimi, Izumbe, Igale ,Njelenje, Ihombe, Isangala, Mlowo, Iwowo, Pashungu, Mbagala, Ilembo, Iwiji na Izyra.

9.2. USHIRIKA/SACCOS.

- i. Idadi ya vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) vimeongezeka kutoka Vyama 28 mwaka 2015 hadi kufikia vyama 29
- ii.Akiba imeongezeka kutoka **Tshs. 3,529,399,946** mwaka 2015 hadi kufikia **Tshs. 3,608,753,520** mwaka 2020 sawa na asilimia 97.8
- Katika kipindi hiki SACCOS imeendelea kuongeza kiasi cha mikopo kinachotolewa kwa wanachama wake kutoka kiasi cha **Tshs. 604,579,450** mwaka 2015 hadi kufikia **Tshs. 3,964,480,250** kwa mwaka 2020
- Vyama vya mazao (AMCOSS) vimeongezeka kutoka vyama 14 mwaka 2015 hadi kufikia vyama vyama 39 mwaka 2020. Aidha vyama hivyo vimeongeza hisa zake kutoka hisa 51,861,000 na kufikia hisa 188,048,500 mwaka 2020.

10.MIFUGO

- **MIRADI YA MAENDELEO SEKTA YA MIFUGO**.

Jumla ya Majosho 5 katika Vijiji vya Iwiji, Mkuyuni, Komondo, Mwela na Nsongwi juu yamekarabatiwa kwa nguvu za wananchi na yanafanya kazi za kuogeshea Mifugo.

ujenzi wa machinjio ya muda ya Utengule Usongwe imekamilika na inafanya kazi ambapo jumla ya **Tshs. 45,765,719.20** zimetumika

10.1 UVUVI

- **Shughuli zisizo za miradi ya maendeleo.**
- Jumla ya Wafugaji 1,624 wamepewa elimu ya mbinu bora za ufugaji samaki ikiwa ni pamoja na uchimbaji mabwawa katika kijiji cha Shamwengo na Utengule Usongwe lishe na uvunaji samaki .

- **Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa;**

Ujenzi wa Kituo 1 cha kuzalisha vifaranga wa samaki kimeanzishwa na sekta binafsi katika kijiji cha Shamwengo

Ujenzi wa Mabwawa ya kufugia samaki yameongezeka kutoka mabwawa 450 mwaka 2015 hadi 761 mwaka 2020 katika vijiji mbalimbali; Izyra 13,Galijembe 3, Ikukwa 3, Mwala 30, Iyunga Mapinduzi 23, Shilanga 58, Mshewe 28, Mbawi 65, Ruanda II 39, Masyeta 20, Mbagala 64, Muvwa 29, Pashungu 36, Itete 3, Izumbwe II 12, Isinde 4, Ikumbi 2, Idiga 4, Iwowo 21, Igalukwa 15, Ijombe 4, Shamwengo 103, Itimba 18, Utengule 25, Itizi 31, Mpande 17, Lwanjilo 7, Mwakasita 12, Nsalala 9, Songwe 5, Imezu 2, Isongole 31 na Sanje 25.

11. ARDHI NA MALIASILI;

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.

Idadi ya viwanja vilivyopimwa imeongezeka kutoka 742 mwaka 2015 hadi 1,456 Mwaka 2020 kati ya hivyo ni viwanja 429 vilivyo pata hatimiliki, vyenye gharama ya **Tsh. 118,869,754.23**

KITENGO CHA NYUKI

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kupitia kitengo cha Nyuki imeendelea na kufanya uhamasishaji kwa Wananchi ili kujiunga katika vikundi ambapo katika kipindi cha Mwaka 2015 hadi Mwaka 2020 Jumla ya vikundi Saba (7) vilikuwa vimeanzishwa kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii na kupewa mafunzo juu ya ufugaji bora wa nyuki na kiasi cha **Tshs 7,450,000.00** zimetumika

12. KITENGO CHA MAZINGIRA NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU

8.1. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Kitengo cha Mazingira imeboresha huduma ya usafi wa mazingira kwa Kununua trekta na tela lake la kufanyia usafi wa mazingira **Tshs 66,000,000.00** zimetumika.pamoja na kutekeza miradi ya maendeleo idara imefanya kazi zifuatazo;

Uzoaji taka umefanyika katika Mji mdogo wa Mbalizi na Inyala wastani wa tani 47,316 zimesombwa **Tshs 24,759,254.00** zimetumika.

Uboreshaji wa mazingira umefanyika kwa kupanda miti 1300 katika kata ya utengule usongwe kwa kupanda pembezoni mwa barabara ya Mbalizi-Tunduma

Usimamizi wa uhifadhi wa mazingira katika mto mbalizi umefanyika kwa kuzuia shughuli za uchimbaji mchanga katika maeneo hayo kwa kushirikiana na kituo cha polisi Mbalizi na Tazara pamoja na viongozi wa Kata na Vitongoji

Shughuli imefanyika katika maeneo ya Kata ya Mshewe na utengule usongwe ikihusisha shule 13 zilizopo mwambao wa mto Nzovwe na jamii iliyopo pembezoni mwa mto Nzovwe katika umuhimu wa utunzaji wa vyanzo vya maji

Kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya Kata na kupitia na kuangalia maeneo kama kuna uvamizi uliofanyika baada ya katazo

Elimu imetolewa kwa wananchi na wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Ileya pamoja na kutembelea machimbo ya mchanga yaliyopo Kijiji cha Nsongwi juu

Kuunda na kufufua Klabu za mazingira katika shule za msingi na sekondari kwa kushirikiana na wadau wa Bonde la ziwa Rukwa, ambapo Elimu imetolewa juu ya uundaji wa klabu katika shule za msingi za Mshewe, Muvwa, Igunga, Iwanga, Utengule, Itimba, Idungumbi, Iwala, na shule za sekondari za Maghabe, Ushindi, St. Mary, Loila na Ilunga zilitembelewa

13. VIWANDA NA BIASHARA.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kupitia Kitengo cha Biashara imeweza kupata mafanikio yafuatayo kwa kipindi cha mwaka 2015 – 2020 kama inavyoonekana kwenye jedwadi hapa chini.

Jedwali Na 5 : Viwanda.

NA.	AINA YA KIWANDA	MWAKA 2015	MWAKA 2020
1.	Vikubwa	1	-
2.	Kati	-	-
3.	Vidogo	32	24
4.	Vidogo sana	50	21
	JUMLA	**83**	**45**

Jedwali Na 6: Leseni za Biashara

NA.	MWAKA 2015	MWAKA 2020
1.	2051	2156

Jedwali Na 7:Leseni za Vileo

NA.	MWAKA 2015	MWAKA 2020
1.	321	297

Jedwali Na 8: Wajasiriamali Wadogo

NA.	MWAKA 2015	MWAKA 2020
1.	5442	5050

14.0 MIUNDOMBINU YA BARABARA

Halmashauri ya Wilaya Mbeya kwa kushirikiana na wakala wa Barabara vijijini (TARURA), tumeweza kufanya matengenezo na ujenzi wa barabara mbalimbali ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na mazao katika wilaya yetu na kuhakikisha barabara zetu zinapitika wakati wote

wa kiangazi na Masika. Kazi hizi zimefanyika/Zinaendelea kufanyika katika maeneo mambilimbali kama inavyoonekana kwenya (***kiambatisho D.*** **63-65)**

15.0 KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi Mwaka 2019/2020

Jedwali Na 9:Hati			
MWAKA	**HATI ILIYOTOLEWA**		
2015/2016	HATI SAFI		
2016/2017	HATI SAFI		
2017/2018	HATI SAFI		
2018/2019	HATI SAFI		

16. KITENGO CHA TEHAMA

Kwa kipindi cha muda wa miaka mitano mwaka 2015/2016 hadi 2019 /2020 Kitengo cha Tehama kimefanya shughuli za miradi kama

- Kusajili,kusanidi,kuhuisha na kusanikisha mfumo wa ukusanyaji wa Mapato kwa njia ya Kielectroniki zikiwemo mashine za POS 154.
- Kufunga mtandao kiambo katika Majengo 5 ya Halmashauri (Jengo la Mkuu wa Wilaya,kituo cha afya Inyala,kituo cha afya Ilembo,Hospitali ya wilaya na Ofisi za Mamlaka ya mji mdogo Mbalizi na kuhudumia miundombinu ya TEHAMA ndani ya Halmashauri.
- Kutengeneza tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya **(www.mbeyadc.go.tz)**
- Kufungua kurasa 4 za mitandao ya kijamii kwa ajili ya kuhabarisha jamii mambo mbalimbali yanayotekelezwa katika Halmashauri.Kurasa hizo ni (Twitter,Youtube,Facebook na Instagra

MIRADI YA KIMKAKATI

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imewekeza kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo ni sehemu ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato. Miradi hiyo iliyotekelezwa ni kama Ifuatavyo;

Ujenzi wa stendi ya mabasi Mbalizi ambayo ni kutekeleza Ahadi ya Mweshimiwa Rais wa Jamuuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli** iliyogharimu **Tshs. 265,000,000** toka mapato ya ndani mradi umekamilika kwa asilimia 95.

Ujenzi wa soko la Tunduma road eneo la Nsalala ambalo mpaka sasa limegharimu jumla ya **Tshs. 78,278,000** toka mapato ya ndani mradi umekamilika kwa asilimia 90.